# Fasihi simulizi

1. Uongozi wa kusahihisha 102/3 (Fasihi)

a) Bembelezi (lal mtoto). Wimbo unambembeleza motto alalye alama 2

b) Sifa za wimbo

- Huimbwa na walezi wa motto
- Huimbiwa watoto wachanga
- Huimbwa kwa sauti nyororo
- Huonyesha hisia za mlezi
- Maneno hurudiwa rudiwa
- Mdundo na taratibu
- Vifungu vifupi vifupi hutumiwa
- Huambatana na kumpapasa papasa motto kwa upole
- Huhusisha watoto wazazi
- Humpatia motto matumaini ya kumwona motto

c) Umuhimu wa wimbo huu

- Hufunza utamaduni
- Hufunza lugha ya ulezi/ mama
- Huliwaza motto mama akiwa mbali
- Hubembeleza motto alale
- Hufunza kuhusu amali ya jamii k.m chakula n.k.
- Mlezi hutoa malalamiko yake
- Hufunza motto mahusiano ya watu

d) Amali za jamii zinazojitokeza

- Vyakula k.v nyama, mkate, ndizi n.k
- Biashara, sokoni
- Ukulima wa ngano (mkate), mgomba (ndizi) Zozote 2x1=2

e) Mbinu zilizotumika

- Kiashiri
- Takriri
- ufafanuzi-1

f) Vitendo ambatano

- Kupapasa motto
- Mlezi hutembea tembea
- Tikisa motto
- Beba motto mgongoni/ begani/ kifuani

g) Wahusika

- Wawili
- Mtoto wa mlezi

2. . a) i)Kisasili

ii) Inaeleza jinsi kifo kilivyoingia duniani

- Asili ya kifo alama 2

b) Sifa za ngano

- Mwanzo maalum (fomula) hapo zamani za……..
- Wahusika wanyama mfano mjusi na kinyonga
- Wanyama kuwasilisha tabia na hisia za binadamu mfano kuongea, kujibizana n.k.
- Tanakali za sauti m.f pu! Zozote 3x1=3

c) Kinyonga ni

- Mvivu/ mzembe/mlegevu
- Si mzingativu- anachelewesha ujunmbe
- Mtiifu- mwishowe alifikisha ujumbe zozote 3x1=3

d) Umuhimu wa hadithi
- Kuelezea asili ya binadamu
- Asili ya kifo
- Huipa jamii melekeo
- Hukumbusha jamii
- Huburudisha/ huliwaza
- Ni historian a utamaduni wa jamii
- Huonya/ huadhibu zozote 4x1=4

e) Njia za kusanya fasihi simulizi
- Mahojiano yaliyopangwa na mtafuti na wahojiwa wake
- Kutumia vinasa sauti
- Kutumia video
- Kwa kuandika data au kazi husika zozote 4x1=4

f) Tambulisha vipera
- Kula hepi- msimu(kuwa na haraka)
- Sema yako ni ya kuazima- msemo (mtu asiringe)
- Baba wa taifa – lajabu (kiongozi wan chi)

3 a) - Huiwasilishwa kwa njia ya mdomo.
- Huhitahi uwepo hadhira
- Huweza kubadilishwa kulingana na hadhira/mahitaji
- Huandama na matendo
- Unaweza kuamba tanishwa na (3X1) ala. 3

b) - Wawe: nyimbo za kilimo (ala. 1)
Kimai: Nyimbo zinazohusiana na shughuli za uvuvi (ala. 1)
Faida:
Kuhimiza bidii.
Shukura kwa mavuno.
Beza uzembe.
Kuchapua utendakazi. ( zozote 2x1 ala. 2)

c) - Huwa na Mdundo| Mahadhi.
-Hupangwa kibeti.
-Hutumia lugha ya mkato.
-Matumizi mengi ya istiari. (zozote 3x1 ala 3.)

d) - Huwa ni fumbo|swali
-Humuia lugha iliyojaa sitiari.
-Ina fomula ya uwasilishaji.
-Huhusisha makundi mawili| watu wawili. (zozote 3x1 ala 3.)

e) i) Istiari
i) Jazanda |Nasiha (ala.1)

f) Matatizo
Watu wanaendelea kuhamia mijini

Dini zinakashifu baadhi ya tamaduni.
Wazee waliohifadhi kumbukumbu hizi wanaendelea knadimika.

Mapendekezo (3x1) ala.3

- Kuborehs zaidi mashidnano katika tamasha za muziki za shule.
- Kuhifadhi kwenye kanda
- Tuwe na makazazi inayoshughul;ikia tamaduni ( 3X1) ala. 3

4. (a)Madhila ya Muitalia (al. 4) ".
- Yeye aliwanyang'anya mashamba wenyeji".
- Walikuwa wabaguzi wa rangi
- Mwafrika alidunishwa
- Mlowezi alikuja mika mingi na amekataa kuondoka katika nchi ya mwafrika".
- Mifugo ya wenyeji inateseka kwa njaa na imekonda mno. Vifaranga, mbuzi n.k".

(b) Sifa za wimbo ".
- Urari katika vina haupo
- Mizani katika mishororo haina urari
- Mishororo katika kila ubeti haijagawanywa kwa ukwapi na utao
- Katika ubeti wa pili wanasema wazee kwa vijana waliimba

(c) Maana ya vifungu (al.4)
(i) Mbavu zao zahesabika
- Mifugo wamekonda mno
- Wamekosa malisho (al. 2)
(ii) - Haya yote hakika, ni madhila ya Muitalia.
- Haya ni mateso/masaibu/matatizo yanayotokana na mlowezi Muitalai ".

(d) - Aina ya wimbo (al.2)
- Wimbo wa ukombozi/uzalendo
- Wenyeji wanaimba na kuonyesha cheche za kutaka kujikomboa kutokana na dhuluma madhila ya walowezi (Waitalia) (kutaja al.1, maelezo al. 1= al.2

(e) Shughuli za kiuchumi(al.2)
(i) Ni wakulima wa mifugo
- Hufuga kuku na mbuzi
(ii) Ni wakulima wa mimea
- Mashamba ambayo wako nayo wanayatumia kwa kilimo cha mimea mbalimbal 2x1=al.2)

(f) Mbinu za lugha (al.2)
(i) Methali- Maji ukiyavulia nguo, ni lazima uyaoge
(ii) Tanakali ya sauti/uidaa/siyahi
Meee !
uui !
Maswali ya balagha /mubalagha
Muitalia alikuja lini ?
Na ataondoka lini ?
a. Takriri – Hatuchoki

(g) Mafunzo katika wimbo
-Mkoloni/ mlowezi, muitalia alipokuja vbarani Afrika aliwakandamiza waafrika kwa mengi
- Umoja wa mwafrika ndio uilioweza kumwondolea dhuluma dhidi ya wanyanyasaji
- Dhuluma in mwanzo na mwisho wake

(viii) Majengo yasiyozingatia viwango vya usalama;
- Bweni la wanafunzi lilikuwa limekomelewa kwa nje
- Madirisha ya bweni yalikuwa yamewambwa kwa vyuma/nyaya kwa madai ya usalama wa wanafunzi
- Shule na hasa bweni kukosa vifaa vya kupambana na moto".

-

5. a) Maana ya mivigo na inakotumika

Mivigo ni sherehe au/ bada zinazofuata utaratibu Fulani wa kisanaa za maonyesho ya fasihi simulizi Al. 1

Inakotumiwa

i. Katika matanga miviga hutumiwa kuliwaza waliofiwa
ii. Katika jando na unyago, makunguni, maghariba na manyakanga hutumia miviga kufunza wavi, nasaha na mazingira yao
iii. Katika mavuno miviga hutumiwa kutoa shukrani
iv. Baada ya vita – hutumiwa kuongoa na kuwatolea shukrani mashujaa waliotoka vitani
v. Motto anapozaliwa au kupewa jina, miviga ya kumkaribisha ilifanywa
vi. Wakati wa arusi
vii. Matambiko ya kutakasa n.k. k.m. aliyemuua mtu
viii. Kutawaza kwa viongozi

b) Sifa za Miviga

Hulenga kundi maalum katika jamii
Hutoa mawaidha
Hukusanya wanaotoa mawaidha na wanaotolewa hayo mawaidha
Hutokea kwa misimu
Kila tukio (jambo) huwa na mivigo yake
Hutumia pesa katika

c) Onyesha umuhimu wa Miviga

Hudumisha mila na utamaduni wa jamii
Huwawezesha vijana kuwa na kumbukumbu za kila sherehe ilivyofanywa, wakati na maana yake
Huelimisha vijana
Hutahadharisha kuhusu maovu
Huwezesha vijana kuelewa au kufahamu desturi zake
Huleta umoja na ushirikiano katika jamii
Huburudisha
Hufundisha unyumba na malezi
Uhimiza bidii ya kufanya kazi na kujitegemea
Huleta maendeleo

6. (a) Ni tungo zilizoundwa kwa mpangilio wa maneno au sauti zilizoteuliwa na msani na zenye utaratibu za kimuziki zinazopanda na kushuka (al. 2)

(b) (i)Tenzi – nyimbo za kutoa mawaidha
(ii) Kongozi – ziliimbwa wakati wa kuaga mwaka
(iii) Sifu – zinaotoa sifa kwa wahusika kutokana na umaarufu
(iv) Wawe – zinazoimbwa na wakulima wakiwa shambani
(v) Tendi – Za masimulizi ya mashujkaa (al.5)

(c)- Huhifadhi matukio muhimu ya kihistoria
- Chombo cha kupitisha utamaduni
- Ni burudani inayotumbuiza waimbaji / hadhira
- Huliwaza na kufariji wenye majonzi
-Huhamasisha watu kushiriki katika kutenda mambo fulani
- Ni njia ya kujipatia kipato
- Hudumisha/huwasilisha usanii wa tamaduni za jamii mbalimbali
- Huelimisha, huonya, husimanga (zozote 5)

(d) BEMBELEZI

- Ziliimbiwa watoto ili watulie/wanyamaze

- Ziliimbwa na walezi /wazazi hasa mama
- Sauti ni ya kubembeleza
- Hutoa ahadi mbalimbali kwa mtoto
- Huwa fupi / hurudiwa –rudiwa
- Ziliburudisha watoto (zozote 5 =al. 5)

7. (a) – Hizi ni hadithi zinazotumia wanyama kama wahusika (mnyama anaweza kusemezana na binadamu)

(b) – Huwezesha fanani na hadhira yake kusema mambo ambayo kwa kawaida ingekuwa mahali/aibu kuyatamka hadharani (kusema kitasifida)

- Ni njia ya pekee ya kufunzia maadili na amali za jamii (kuyapigia mambo chuku)
- Kutahadharisha hadhira dhidi ya watu waovu katika jamii (Sungura na Fisi ujanja wao ni sawa na matapeli)
- Hufurahisha . Hii ni kwa sababu, nyingi ya hadithi hizi huchekesha na kuleta huruma kwa wengine (Sungura kupigana na Ndovu na kumshinda ni kichekesho)

(c) – Watu wazima kuwasimulia watoto

- Watoto kusimuliana hadithi wenyewe kwa wenyewe
- Watu wazima kusimulia mseto wa watu wazima na watoto
- Watoto kusimulia hadhira ya mseto wa watu wazima na watoto

8. (a)(i) Fasihi ya ngoma

(ii) Matumizi ya ala

Hakuna sauti ya binadamu

Mdundo hotoa ujumbe fulani

Hutumiwa kw anjia ya mawasilinao

Saiuti ni ya kupasha ujumbe (zozote 2x1=al. 2)

Wapigaji ngoma na ala zingine

ni watu teule katika jamii

(b) (i) Hurafa- Wahusika ni wanyama

Hekaya- ujanja, ucheshi , werevu an ushindi hujitokeza al.2)

(ii) Visasili /ngano za zuli – hutoa maelezo kuhusu asili ya hali fulani

- Hujibu swali kwa nin kitu fulani kiko jinsi kilivyo
- Visakale – visa vya kale vya mashujaa /majagina (migani)

(iii) Mtanziko – Ngano zinazomwacha msomaji/ mhusika katika hali ya kutojua achague lipi.

- Ni msimulizi huuliza swali

Mazimwi – Hadithi za majitu za kuogofya

- Kiumbe cha kufikirika akilini

(c) (i) Vitendawili – tungo fupi inayotoa maelezo yanayoishia kwenye swali

(ii) Mbinu – Takriri

- Istiara\- Ukinzani

_ Tanakali ya sauti (zozote 4x1= al. 4)

9. a) i)

- Tumbuizo – wimbo wa kuburudisha katika hafla ya arusi
- Wimbo wa kitamaduni

ii) Kuumeni – wanaume

Kukeni – wanawake

Wanaume wanawakilisha wakwe na Tausi (anayeolewa) na wanawake wanawakilisha wazazi wa Tausi

iii) - Watu wa kukeni wana moyo wa kisebusebu na roho kipapo. Walipenda mtoto wao aolewe lakini awaondokeapo na kwenda kwa mumewe waliona

uchungu, kwani walijua huduma alizokuwa akiwapa tausi, zingekoma mara moja
- Upande wa kuumeni walifurahi kwani walijua Tausi angeongezea huduma upande wao

iv) – Unaburudisha waliofika kwenye sherehe ya arusi
- Unaleta ushirikiano baina ya pande mbili
- Unatoa ujumbe kuwa kuondoka kwa mtu mliyezoena huwa ni wakati mgumu sana

v) takriri – Kurudia maneno kwa madhumuni ya kusisistiza mfano kisura wetu,

b)

- Mbolezi – nyimbo za matanga
- Bembelezi – kunarai watoto walale
- Hodiya/ kazi – wakati wa kazi
- Nyimbo za kitaifa – kuonyesha uzalendo kwa taifa
- Nyimbo za kisiasa – kumsifu au kumkejeli kiongozi wa kisiasa
- Nyimbo za kidini – katika ibada
- Vichapuzi – nyimbo zinazoandamana na usimulizi

10. a) i) Sifa za Hurafa
- Ni hadithi
- Wahusika aghalabu huwa wanyama
- Hupewa sifa na matendo ya binadamu
- Huwa na mafumbo Zozote 2x1=2

ii) Sifa za Mighani
- Ni hadithi za mashujaa
- Ni hadithi za kihistoria
- Wahusika huwa mashujaa
- Hupigania haki za wanyonge Zozote 2x1=2

iii) Sifa za Miviga
- Hujumuisha vitendo maalum k.v. kuimba, kuruka, kucheza ngoma
- Huhusisha maombi
- Aghalabu wahusika hutoa sadaka
- Wahusika huweka ahadi (kiapo)
- Kuna matumizi ya vifaa, mavazi na mapambo maalum Zozote 2x1=2

b) Umuhimu wa Ngomezi
- Hutoa taarifa kwa njia nyepesi na kuwafahamisha wanajamii kuhusu matukio Fulani k.v. sherehe, mkutano
- Hutumika kutahadharisha watu
- Hutumika kutoa matangazo rasmi
- Ni njia ya kudumisha utamaduni
- Ni njia ya kudhihirisha ufundi wa jamii 5x1=5

Umuhimu wa mafumbo
- Huburudisha
- Huonya na kutoa mawaidha
- Huimarisha uwezo wa kiakili
- Hufikirisha
- Huimarisha usikivu na uwezo wa kukumbuka
- Hukuza lugha Zozote 5x1=5

Tofauti kati ya malumbano ya utani na mawaidha

| Mawaidha | Malumbano ya utani |
|---|---|
| i) Hutolewa na watu maalum katika jamii | i) Wahusika hukubaliana kufanyiana utani |

| | |
|---|---|
| ii) Hutolewa na wakubwa kwa wadogo<br>iii) Mawaidha hutumia lugha ya kipekee ya kuathiri na kuvuta nadhari | ii) Hutokea kwa njia ya malumbano au kujibizana<br>iii) Mtani hutumia lugha ya ucheshi na upigaji chuku Zozote 2x2=4 |

12. i) Maana ya vitanza ndimi

Ni maneno ambayo hutatanisha wakati wa kutamka kwa sauti ambazo zinafanana

ii) Kumzoesha anayetamka ufasaha wa kuyatamka maneno

Kueneza maarifa kuihusu lugha Fulani

Kufikirisha hasa kuielewa maana ya kitanza ulimi kinachohusika

Kuujenga uwezo wa kuongea au kuzungumza bila ya shida

Kuendeleza utamaduni kwa kurithishana maarifa ya sanaa folklore

Kuwanoa wanajamii ambao baadaye watakuwa na ugwiji wa ulumbi alama 8